JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TATU

27 APRILI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TATU TAREHE 27 APRILI, 2017

I. DUA:

Dua ilisomwa saa 3:00 asubuhi na Mhe. Dkt. Tulia Ackson aliongoza Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Charles Mloka
2. Ndugu Ramadhani Issa
3. Ndugu Lawrence Makigi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

(i) Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(ii) Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iii) Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

III. MASWALI YA KAWAIDA

OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali Na. 105: Mhe. John Peter Kadutu

Nyongeza: Mhe. John Peter Kadutu
Mhe. Joyce J. Mukya
Mhe. Ritta E. Kabati

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 106: Mhe. Othman Omari Haji

Nyongeza: Mhe. Othman Omari Haji
Mhe. Martha J. Umbulla
Mhe. Peter A. Lijualikali
Mhe. Abdallah Hamis Ulega

Swali Na. 107: Mhe. Esther Nicolaus Matiko
Nyongeza: Mhe. Esther Nicolaus Matiko
Mhe. Shaban O. Shekilindi
Mhe. Pascal Y. Haonga

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 108: Mhe. Asha Abdullah Juma

Nyongeza: Mhe. Asha Abdullah Juma
Mhe. Yusuf Hussein
Mhe. Joseph K. Musukumu
Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa

Swali Na. 109: Mhe. Godfrey William Mgimwa

Nyongeza: Mhe. Godfrey William Mgimwa
Mhe. Lucy M. Mlowe
Mhe. Sixtus R. Mapunda

MATANGAZO:

WAGENI

Mhe. Naibu Spika alitangaza wageni wote waliotufikia na kuhudhuria Bunge kuwa ni pamoja na wageni wa Mhe. Prof. Mbarawa Makame (Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano).

Mgeni wa Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sana na Michezo kwa mshindi wa medali ya dhahabu katika mbio za Ndugu Alphonce Simbu.

Wageni wa Mhe. Margareth Sitta kutoka D'Salaam.

Wageni 100 wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Mwigulu L. Nchemba na wageni wengine mbalimbali.

IV. TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Naibu Spika alitoa taarifa ya Spika kuhusu mwongozo wa Mhe. Dotto Biteko aliyetaka kujua kuhusu mauaji ya Polisi 8 na kuiomba Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kulifanyia kazi. Hivyo, Kamati hiyo imefanya Kikao na kumwita Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na sasa tayari taarifa imewasilishwa kwa Spika.

V. MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Bilago Kanuni 64(7) alitaka kujua kama Sikukuu inapoangukia siku ya Jumatano na kunakuwa hamna maswali kwa Waziri Mkuu kwa sababu Wabunge hawakuweza kujiorodhesha sasa kama ikitokea sikukuu nyingine zitaangukia Jumatano Wabunge watapoteza haki yao ya kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu.

   Mhe. Naibu Spika alitoa mwongozo kwamba kwa kuwa Mhe. Bilago hana uhakika kuna siku ngapi zinaangukia siku ya Jumatona hivyo hana haja ya kuutolea mwongozo.

2. Mhe. Esther Matiko kwa kutumia Kanuni 68(7) alitaka kujua kwa nini askari Magereza hawalipwi posho inayojulikana kama *package allowance* ambaye askari wenzao wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Polisi wanalipwa kwa nini kuna ubaguzi.

   Mhe. Naibu Spika alitoa mwongozo kwamba kwa kuwa suala hilo halijatokea humu ndani hawezi kulitolea mwongozo ila hata hivyo Serikali imesikia kuhusu suala hilo.

3. Mhe. Joseph Musukuma kuhusu Kanuni 68(7) na 64(e) (g) kwamba Wabunge wengi wa Zanzibar wanaposimama mara nyingi humu Bungeni wanasema hawamtambui Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Shein kwa nini suala hilo lisisemwe nje ya Bunge na sio humu ndani.

   Mhe. Naibu Spika alitoa mwongozo kwamba Wabunge wazingatie Kanuni za Bunge ili wasiseme maneno ambayo yatadhalilisha Viongozi wetu.

4. Mhe. Sofia Mwakagenda kwa kutumia Kanuni 68(7) ambaye alitaka kujua kwa nini Serikali wakati wa kujibu masuala yanayojibiwa kisiasa badala ya kujibu kikamilifu. Alitoa mfano wa swali 106 ambapo pia katika kujibu kama swali limeulizwa na Kambi ya Upinzani katika kujibu anamtaja Mbunge wa Chama cha Siasa badala ya kumjibu Mbunge alieuliza swali.

   Mwongozo wa Spika ni kwamba Mawaziri wazingatie uzito wa maswali na wajibu kikamilifu na ajibiwe Mbunge aliyeuliza swali na sio vinginevyo.

5. Mhe. Dkt. Suleiman kwa kutumia Kanuni 68(7) alitaka kujua kwamba Naibu Waziri wakati anajibu swali 106 ametoa shutuma nzito za uongo kwamba Viongozi Waandamizi wa CUF walienda kuchoma nyumba na alimtaka Mhe. Naibu Waziri kuleta ushahidi.

Mwongozo wa Naibu Spika ni kwamba kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge anayetakiwa kuleta ushahidi sio yule anayetuhumiwa bali msemaji alisema Mbunge fulani anasema uwongo hivyo yeye ndiyo anayetakiwa kuleta ushahidi hata hivyo kwa sababu tupo katika kujifunza leo hatotaka maelekezo ya kuleta ushahidi.

VI. HOJA ZA SERIKALI

1. Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Mhe. Naibu Spika alimwita mtoa hoja Mhe. Prof. Mbarawa Makame, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuwasilisha hoja yake.

2. Mhe. Prof. Norman A. Sigalla King, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

3. Mhe. Mary M. Mwanjelwa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira aliwasilisha Taarifa na maoni ya Kamati hiyo kuhusu (Mazingira).

4. Mhe. David Ernest Silinde aliwasilisha Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Baada ya shughuli za kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kukamilika Mhe. Naibu Spika alianza kuwaita wachangiaji kama ifuatavyo:-

   (3) Mhe. Mariam Kisangi - CCM

   Aidha, kabla ya kuanza kuchangia Mhe. Naibu Spika alitoa ufafanuzi na marekebisho kwamba Ndugu Alphonce

Simbu wiki iliyopata mashindano ya London Marathon alishika nafasi 5 na mapema mwaka huu alipata medali ya Dhahabu huko Mumbai.

(4)	Mhe. Dkt. Prudenciana W. Kikwembe	-	CCM
(5)	Mhe. Peter J. Serukamba	-	CCM
(6)	Mhe. Latifa Hassan Chande	-	CHADEMA

VII. KUSITISHA BUNGE

Shughuli za Bunge zilisitishwa saa 6:55 mchana hadi saa 11:00 jioni.

VIII. BUNGE KURUDIA

Baada ya mapumziko ya mchana Shughuli za Bunge zilirudia saa 11:00 zikiongozwa na Naibu Spika. Waheshimiwa Wabunge wafuata waliendelea kuchagnia kama ifuatavyo:-

(7)	Mhe. Augustino Manyanda Masele	-	CCM
(8)	Mhe. Mbaraka Kitwana Dau	-	CCM
(9)	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	CCM
(10)	Mhe. Mary Deo Muro	-	CHADEMA
(11)	Mhe. Rioba Marwa Chacha	-	CHADEMA
(12)	Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab	-	CCM
(13)	Mhe. Rita Enespher Kabati	-	CCM
(14)	Mhe. Mussa Bakari Mbarouk	-	CUF
(15)	Mhe. Vedasto Edgar Ngombale	-	CUF
(16)	Mhe. Cecil David Mwambe	-	CHADEMA
(17)	Mhe. Hasna Sudi Mwilima	-	CCM
(18)	Mhe. Ezekiel Magolyo Maige	-	CCM
(19)	Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq	-	CCM
(21)	Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby	-	CCM
(22)	Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma	-	CCM
(23)	Mhe. Hongoli Ismail Joram	-	CCM
(24)	Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa	-	CCM
(25)	Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa	-	CCM
(26)	Mhe. Maganlal Meisuria Bhagwanji	-	CCM

IX. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE

Shughuli za Bunge ziliahirishwa saa 1:45 usiku hadi kesho tarehe 28 Apirli, 2017 saa 3:00 asubuhi.